

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA  
BUNGE LA TANZANIA**

Tele: +255 0262322761-5  
Fax No. +2550262324218  
**Email:**[info@bunge.go.tz](mailto:info@bunge.go.tz)



Ofisiya Bunge  
S.L.P 941  
**DODOMA**

**TAARIFA KWA UMMA**

Spika wa Bunge Mheshimiwa Job Ndugai amemuandikia Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), Mheshimiwa Jaji Mstaafu Semistocles Kaijage kumfahamisha kuwa Jimbo la Singida Kaskazini liko wazi baada ya aliyekuwa Mbunge wa Jimbo hilo Ndg. Lazaro S. Nyalandu kufutwa uanachama na Chama cha Mapinduzi (CCM) tarehe 30 Oktoba 2017.

Mheshimiwa Spika ameandika barua hiyo kwa mujibu wa kifungu 37(3) cha Sheria ya Taifa ya Chaguzi (Sura ya 343, ya mwaka 2015) kinachoelekeza kwamba, pale ambapo Mbunge, atajiuzulu, atakufa au sababu nyingine yeyote tofauti na zilizoainishwa katika kifungu cha 113, Spika atamjulisha Mwenyekiti wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi na kutangaza kwenye Gazeti la Serikali kwamba kiti hicho cha Ubunge kiko wazi.

Kufuatia barua hiyo Tume ya Taifa ya Uchaguzi, inaweza kuendelea na mchakato wa kumpata Mbunge wa kujaza nafasi hiyo iliyowazi ya Jimbo la Singida Kaskazini.

**Imetolewa na:** Kitengo cha Habari Elimu kwa Umma na Mawasiliano  
Ofisi ya Bunge  
S.L.P. 941  
**DODOMA**

03 Novemba 2017